# BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

## TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA TATU MWAKAA 2023

## 208 KIARABU

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ............................................................................................. 1

2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ..................................................................... 1

3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ..................... 1

3.1 SEHEMU A: KUSOMA, UFAHAMU NA UFUPISHO ..................................... 1

3.1.1 Swali la 1: Ufahamu ............................................................................. 1

3.1.2 Swali la 2: Ufahamu ............................................................................. 4

3.1.3 Swali la 3: Ufupisho wa habari ............................................................. 7

3.2 SEHEMU B: MATUMIZIYA LUGHA ............................................................ 9

3.2.1 Swali la 4: Matumizi ya lugha ............................................................... 9

3.2.2 Swali la 5: Matumizi ya lugha ............................................................. 12

3.2.3 Swali la 6:Matumizi ya lugha .............................................................. 14

3.2.4 Swali la 7: Matumizi ya lugha ............................................................. 16

3.2.5 Swali la 8:Matumizi ya lugha .............................................................. 18

3.3 SEHEMU C: KANUNI ZA LUGHA NA SARUFI(ةيوغللا دعاوقلا)))) ................ 19

3.3.1Swali la 9: Kanuni za lugha na Sarufi .................................................... 19

3.3.2 Swali la 10: Kanuni za lugha ............................................................... 21

3.3.3 Swali la 11:Kanuni za lugha ................................................................ 23

3.3.4 Swali la 12: Kanuni za lugha ............................................................... 25

3.4. SEHEMU D: UTUNGAJI(ريبعتلا)) ............................................................. 27

3.4.1 Swali la 13: Utungaji .......................................................................... 27

3.4.2 Swali la 14: Utungaji .......................................................................... 30

4.0 HITIMISHO ............................................................................................. 33

5.0 MAPENDEKEZO ...................................................................................... 33

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa mtihani wa kuingilia Kidato cha Tatu katika somo la Kiarabu mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa kuingilia Kidato cha Tatu ni mtihani ambao unakusudia kupima ni kwa kiasi gani watahiniwa wamejifunza kupitia miaka miwili ya sekondari ya awali. Kupitia matokeo ya mtihani huu, watahiniwa hupokea matokeo hayo yanayowaonesha ufaulu wao kwa lengo la kuweza kuendelea na ngazi nyengine ya elimu au kutoendelea.

Uchambuzi uliowasilishwa katika ripoti hii, unakusudia kuonesha tathmini juu ya majibu ya Watahiniwa katika somo la Kiarabu. Ripoti inabainisha sababu tofauti zilizosababisha watahiniwa kujibu vizuri au vibaya. Miongoni mwa sababu za watahiniwa kufanya vizuri ni kufahamu swali linatakiwa lijibiwe vipi, uwezo waliokuwa nao kwa baadhi ya watahiniwa kujieleza katika lugha ya Kiarabu na kuweza kuelewa kanuni za lugha na sheria zake.

Aidha, watahiniwa walijibu vibaya baadhi ya maswali kwa sababu zifuatazo, kushindwa kufahamu swali linatakiwa lijibiwe vipi, uwezo mdogo wa kujieleza katika lugha ya Kiarabu na uchache wa kuelewa kanuni za lugha na sheria zake.

Kwa kuendelea zaidi, uchambuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia chati ambazo zimebainishwa kwa rangi tofauti. Chati hizo zinaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, ni imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiarabu kwa mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**Dkt. RASHID A. MUKKI**



**MKURUGENZI**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**ZANZIBAR**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha ufaulu wa mtihani wa kuingilia Kidatu cha Tatu kwa somo la Kiarabu mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Taifa wa mwaka 2010 na kufuata muundo wa mtihani wa Kidato cha Pili wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2015.

Mtihani wa Kiarabu ulilikuwa na maswali kumi na nne (14) yaliyogawanywa katika Sehemu A, B, C na D, kwa kuzingatia mada ya Ufahamu, Kanuni za Lugha, Matumizi ya Lugha na Utungaji. Watahiniwa walitakiwa wajibu maswali yote katika kila sehemu, isipokuwa sehemu D walitakiwa kujibu swali moja tu, Hivyo jumla ya maswali waliyotakiwa kujibu watahiniwa yalikuwa 13 kati ya 14 yaliyoandikwa katika karatasi ya mtihani wao.

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **3,739** sawa na asilimia **18.31** ya watahiniwa **20,422** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 29, wastani 30 hadi 64na vizuri 65 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia chati/grafu kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilishavibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B, C, na D. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa.

### 3.1 SEHEMU A: KUSOMA, UFAHAMU NA UFUPISHO

Sehemu hii ililikuwa na jumla ya alama ishirini na tano (25) zilizogawanywa katika maswali matatu (3), kwa mgawanyo ufuatao:-Swali la kwanza na la pili yalikuwa na alama kumi (10) kila moja (1), na swali la tatu lililikuwa na alama tano (5).Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

#### 1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali la kwanza lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kusoma habari aliyopewa kisha kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo. Swali hili lililikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele (أ) cha swali kilimtaka mtahiniwa kueleze sehemu aliokuwa akiishi simba.

Kipengele (ب)kilimtaka mtahiniwa kuelezea hali aliyokuwanayo simba.

Kipengele (ج) kilimtaka mtahiniwa kutoa sababu iliyopelekea simba asiweze kuwinda wakati alipozeeka.

Kipengele (د) kilimtaka mtahiniwa kueleza alichofanya simba wakati alipokuwa anaumwa.

Kipengele (ه)kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari aliyoisoma.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma habari na kujibu maswali kulingana na habari husika.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,687** sawa na asilimia **9**8.61 na watahiniwa **52** sawa na asilimia **1.39** hawakujibu swali husika.Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.


**Jadweli Nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUM-LA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,682 | 45.62 | 1,769 | 47.98 | 236 | 6.40 | 2,005 | 54.38 |

Takwimu za jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa ufaulu wa asilimia **47.98** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **54.38.**

Aidha watahiniwa **1,682** sawa na asilimia **45.62** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1.

**Kielelezo1.1 (Kibaya)**


أ- أَيْنَ كَانَ يَعِيشُ الأَسَدُ؟

ب- كَيْفَ كَانَ حَالُ الأَسَدِ؟


ج- لِمَاذَا لَمْ يَسْتَطِعِ الأَسَدُ أَنْ يَصْطَادَ لَمَّا شَاخَ؟

د- مَاذَا فَعَلَ الأَسَدُ لَمَّا مَرِضَ؟

هـ- مَا عُنْوَانٌ مُنَاسِبٌ لِلْقِصَّةِ السَّابِقَةِ؟

Kielelezo 1.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vibaya swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakufahamu vizuri habari aliyosoma, hivyo hakuweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu, kwani kanukuu baadhi ya ibara kutoka katika habari aliyosoma na kufanya ndio majibu ya maswali aliyoulizwa.

**Kielelezo 1.2 (Kizuri)**


أ- أَيْنَ كَانَ يَعِيشُ الأَسَدُ؟ كان أسد يعيش في مكان بكثير فيه الشجرة.

ب- كَيْفَ كَانَ حَالُ الأَسَدِ؟ كان الأسد متمتعا محترمة، تهابه كل الوحوش في الغابة لشدة بأسه.

ج- لِمَاذَا لَمْ يَسْتَطِعِ الأَسَدُ أَنْ يَصْطَادَ لَمَّا شَاخَ؟ لأنه كما كان في أيام قوته.

د- مَاذَا فَعَلَ الأَسَدُ لَمَّا مَرِضَ؟ يستطيع أن على إصطياد كما كان في أيام قوته.

هـ- مَا عُنْوَانٌ مُنَاسِبٌ لِلْقِصَّةِ السَّابِقَةِ؟ الأسد مريضا.

Kielelezo 1.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alifahamu vizuri habari aliyosoma, hivyo aliweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu.

**3.1.2 Swali la 2: Ufahamu**

Swali la pili lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kusoma habari aliyopewa kisha kujaza nafasi zilizoachwa wazi. kwa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa jawabu aliyopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kujaza neno lililokosekana katika ibara husika kwa kuchagua jibu au neno sahihi miongoni mwa majibu au maneno aliyopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma habari na kujibu maswali kulingana na habari husika pamoja na umakini wa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa majibu aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,716** sawa na asilimia **99.38** na watahiniwa **23** sawa na asilimia **0.62** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1b.


**Jadweli Nambari1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 524 | 14.10 | 708 | 19.05 | 2,484 | 66.85 | 3,192 | 85.90 |

Takwimu za jadweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **66.85** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri kwa asilimia **85.90.**

Aidha, watahiniwa **524** sawa na asilimia **14.10** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1.

**Kielelezo 2.1 (Kibaya)**


٢- إِمْلَأْ اَلْفَرَاغَاتِ اَلْآتِيَةَ بِوَضْعِ كَلِمَةٍ مُنَاسِبَةٍ مِمَّا بَيْنَ اَلْقَوْسَيْنِ:-

أ- كَانَ أَسَدٌ ______ مُحْتَرِمًا، تَهَابُهُ كُلُّ الْوُحُوشِ (مُتَنَعِّمًا - مُتَمَتِّعًا - مُتَوَحِّشًا)

ب- قَالَ الثَّعْلَبُ أَتَيْتُ لِأَعُودَ سَيِّدَ الْوُهُوشِ. (الْوُهُوشِ - الدُّهُوشِ - الْوُحُوشِ)


ج- أَتَى ثَعْلَبٌ وَوَقَفَ بِـ جِوَارِ الْغَارِ (بَابِ - جِوَارِ - مَخْرَجِ).

د- عَمِدَ الْأَسَدُ إِلَى الْحِلْيَةِ لِتَحْصِيلِ عَلَى غِذَائِهِ. (الهِيلَةِ - الْحِلْيَةِ - الحِيلَةِ).

هـ- مَا لَكَ لَا تَدْخُلُ حَتَّى نَأْتَنِسَ بِكَ فِي الحَالَةِ الْوَحْدَةِ (الحَالِ - الحَالَةِ - الخَالَةِ)

Kielelezo 2.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakufahamu habari aliyosoma, hivyo hakuweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu kwa sababu hakuweza kuchagua majibu sahihi miongoni mwa majibu aliyopewa.

**Kielelezo 2.2 (Kizuri)**



٢- إِمْلأِ اَلْفَرَاغَاتِ اَلْآتِيَةَ بِوَضْعِ كَلِمَةٍ مُنَاسِبَةٍ مِمَّا بَيْنَ اَلْقَوْسَيْنِ:-

أ- كَانَ أَسَدٌ مُتَنَعِّمًا مُحْتَرِمًا، تَهَابُهُ كُلُّ الْوُحُوْشِ (مُتَنَعِّمًا – مُتَمَتِّعًا – مُتَوَحِّشًا)

ب- قَالَ الثَّعْلَبُ أَتَيْتُ لِأَعُوْدَ سَيِّدَ الْوُحُوشِ. (الْوُهُوْشِ – الدُّهُوْشِ – الْوُحُوْشِ)

ج- أَتَى ثَعْلَبٌ وَوَقَفَ بِـ بَابِ الْغَارِ (بَابِ – جِوَارِ – مَخْرَجِ).

د- عَمِدَ الْأَسَدُ إِلَى الحِيْلَةِ لِتَحْصِيْلِ عَلَى غِذَائِهِ.(الهِيْلَةِ – الْحِلْيَةِ – الحِيْلَةِ).

هـ - مَا لَكَ لاَ تَدْخُلُ حَتَّى نَأْتَنِسَ بِكَ فِيْ الخَالَةِ الْوِحْدَةِ (الحَالِ – الحَالَةِ – الخَالَةِ)

Kielelezo 2.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyefanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alifahamu vizuri habari aliyosoma, hivyo aliweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu kwa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa majibu aliyopewa.

### 3.1.3 Swali la 3: Ufupisho wa habari

Swali la tatu lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kusoma habari aliyopewa kisha kufupisha habari hiyo kwa maneno yasiyozidi khamsini (50) bila kupoteza uhalisia wake.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kufupisha habari aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,064** sawa na asilimia **81.95**, watahiniwa **675** sawa na asilimia **18.05** hawakujibu swali hili.Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1c.


**Jadweli nambari 1c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,359 | 44.35 | 1,001 | 32.67 | 704 | 22.98 | 1,705 | 55.65 |

Takwimu za jadweli nambari 1c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **44.35** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **55.65.**


Aidha, watahiniwa **1,359** sawa na asilimia **44.35** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya ufupisho wa habari kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.

**Kielelezo 3.1 (Kibaya)**


٣- لَخِّصِ الْقِطْعَةَ السَّابِقَةَ بِمَا لاَ يَزِيْدُ عَنْ خَمْسِيْنَ كَلِمَةً.

Kielelezo 3.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na uweledi wa kufupisha habari aliyosoma, hivyo hakuweza kufupisha habari hiyo kwa usahihi kama alivyotakiwa kufanya kwani alinukuu baadhi ya maneno ya habari aliyosoma na kufanya ndio ufupisho wa habari hiyo, jambo ambalo limesababisha kutokuwa na maana au kutofahamika kwa ufupisho wake huo.

**Kielelezo 3.2 (Kizuri)**


٣- لَخِّصِ الْقِطْعَةَ السَّابِقَةَ بِمَا لاَ يَزِيْدُ عَنْ خَمْسِيْنَ كَلِمَةً.

Kielelezo 3.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alikuwa na uweledi ama umahiri wa kufupisha habari aliyosoma, hivyo aliweza kufupisha habari hiyo kwa usahihi kama alivyotakiwa kufanya.

## 3.2 SEHEMU B: MATUMIZIYA LUGHA

Sehemu hii ililikuwa na jumla ya maswali matano (5): swali la nne (4) hadi la nane (8) kutoka katika mada ya matumizi ya lugha. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote matano (5) na kila swali lililikuwa na alama tano (5), hivyo inafanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa ishirini na tano (25). Uchambuzi katika sehemu hii kwa kila swali umezingatia viwango vitatu (3) vya ufaulu, ambavyo ni vizuri, wastani na vibaya. Ufaulu mzuri umeanza alama 3 hadi 5, ufaulu wa wastani ulilikuwa ni alama 1.5 hadi 2.5 na ufaulu mbaya ulianza 0 hadi1.

### 3.2.1 Swali la 4: Matumizi ya lugha

Swali la nne lilitokana na mada ya sentensi zenyekuleta maana kamili ambapo mtahiniwa alitakiwa kubadilisha sentensi alizopewa kutoka hali moja kwenda hali nyingine.. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kubadilisha sentensi kutoka«جملة اسمية»kwenda «جملة فعلية»

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uundaji wa sentensi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,813** sawa na asilimia **75.23** na watahiniwa **926** sawa na asilimia **24.77** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.


**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,816 | 64.56 | 179 | 6.36 | 818 | 29.08 | 997 | 35.44 |

Takwimu za jadweli nambari 2a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **64.56** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **35.34.**


Aidha, watahiniwa **1,816** sawa na asilimia **64.56** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kubadilisha sentensi walizopewa kutoka hali moja kwenda hali nyingine kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1.

**Kielelezo4.1 (Kibaya)**


٤- حَوِّلِ الْجُمَلَ الْآتِيَةَ إِلَى الْجُمَلِ الْفِعْلِيَّةِ:


أ- أَنَا كَاتِبُ الرِّسَالَةِ.


ب- الطُّلَّابُ نَجَحُوْا فِي الِامْتِحَانِ.




Kielelezo 4.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na uwelewa mzuri wa kubadilisha sentensi za«ةلمج ةيمسا»na kuzipeleka katika«ةلمج ةيلعف»kwa usahihi kama alivyotakiwa kufanya. Mtahiniwa huyu yeye aliandika «ةلمج ةيمسا» kama ilivyo katika kipengele «أ», kafanya uchambuzi katika kipengele «ب» na kanukuu neno moja moja katika vipengele vitatu vya mwisho.

**Kielelezo 4.2 (Kizuri)**




Kielelezo 4.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali husika, kwani anaonekana kuwa alikuwa na uwelewa mzuri wa kubadilisha sentensi zilizoanza na jina na kuzipeleka katika hali ya kuanza na kitendo.

### 3.2.2 Swali la 5: Matumizi ya lugha

Swali la tano lilitokana na uuundaji wa sentensi zenye kuleta maana kamili ambapo mtahiniwa alitakiwa kupanga maneno aliyopewa ili kuunda sentensi sahihi. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kupanga maneno kwa mujibu wa kanuni na taratibu za lugha ya Kiarabu kwa kuzingatia maana na matumizi sahihi ya lugha ya Kiarabu.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa uundaji wa sentensi sahihi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,705** sawa na asilimia **72.35** na watahiniwa **1,034** sawa na asilimia **27.65** hawakujibu. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2b.


**Jadweli nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,127 | 41.66 | 694 | 25.66 | 884 | 32.68 | 1,578 | 58.34 |

Takwimu za jadweli nambari 2b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **41.66** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **58.34** .

Aidha, watahiniwa **1,127** sawa na asilimia **41.65** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya uundaji wa sentensi kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1.

**Kielelezo 5.1 (Kibaya)**


٥ـ رَتِّبْ كَلِمَاتِ كُلِّ سَطْرٍ مِمَّا يَأْتِي لِتُكَوِّنَ مِنْهَا جُمَلاً مُفِيْدَةً:-

أ - عَلِيٌّ ـــ خُبْزًا ـ اِشْتَرَى ـــ لِأَهْلِ ـــ بَيْتِهِ. … اشترى لأهل علي خبزا بيته

ب - مُمْتِعَةٌ ـ هَذِهِ ـ وَ ـ الرِّحْلَةُ ـ جَمِيْلَةٌ. … الرحلة ممتعة وهذه جميلة


ج - أَنْ ـ أَتَمَنَّى ـ جَيِّدَةٍ ـ تَكُوْنَ ـ بِصِحَّةٍ. … أن تكون بصحة جيدة أتمنى

د - اَلْمَرِيْضَ ـ يُعَالِجُ ـ اَلطَّبِيْبُ. … الطبيب المريض يعالج

هـ - قِبْلَةُ ـ اَلْكَعْبَةُ ـ اَلْمُسْلِمِيْنَ. … الكعبة المسلمين قبلة

Kielelezo 5.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyefanya vibaya swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana hakuwa na uweledi au umahiri wa kuunda sentensi sahihi kwa mujibu wa maelekezo aliyopewa, badala yake yeye alichukuwa maneno hayo na kuyaweka pamoja na kuyapanga alivyotaka yeye bila kuzingatia maana ya maneno hayo katika tungo.

**Kielelezo 5.2 (Kizuri)**


٥ـ رَتِّبْ كَلِمَاتِ كُلِّ سَطْرٍ مِمَّا يَأْتِي لِتَكُوْنَ مِنْهَا جُمَلاً مُفِيْدَةً:-

أ - عَلِيٌّ ـــ خُبْزًا ـــ اِشْتَرَى ـــ لِأَهْلِ ـــ بَيْتِهِ: اشترى علي خبزا لأهل بيته

ب - مُمْتِعَةٌ ـ هَذِهِ ـ وَ ـ الرِّحْلَةُ ـ جَمِيْلَةٌ: هذه الرحلة جميلة وممتعة

ج - أَنْ ـ أَتَمَنَّى ـ جَيِّدَةٍ ـ تَكُوْنَ ـ بِصِحَّةٍ: أتمنى أن تكون بصحة جيدة

د - اَلْمَرِيْضَ ـ يُعَالِجُ ـ اَلطَّبِيْبُ: يعالج الطبيب المريض

هـ - قِبْلَةُ ـ اَلْكَعْبَةُ ـ الْمُسْلِمِيْنَ: قبلة المسلمين الكعبة

Kielelezo 5.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyefanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana alikuwa na uweledi au umahiri wa kuunda sentensi sahihi kwa mujibu ya maelekezo aliyopewa.

### 3.2.3 Swali la 6:Matumizi ya lugha

Swali la sita lilitokana na mada ya aina za maneno ambapo mtahiniwa alitakiwa kujaza au kukamilisha maneno katika sehemu zilizoachwa wazi kwa kuzingatia umoja, uwili na wingi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika aina za maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,626** sawa na asilimia **96.98** na watahiniwa **113** sawa na asilimia **3.02** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2c.


**Jadweli nambari 2c: Uchambuzu wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,287 | 35.49 | 1,264 | 34.86 | 1,075 | 29.65 | 2,339 | 64.51 |

Takwimu za jadweli nambari 2c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **35.49** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa asilimia **64.51.** **.**

Aidha, watahiniwa **1,287** sawa na asilimia **35.49** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya aina za maneno kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1.

**Kielelezo 6.1 (Kibaya)**




٦ـ أَكْمِلِ الْجَدْوَلَ الْآتِيَةَ:-

| مُفْرَدٌ | مُثَنًّى | جَمْعٌ |
|---|---|---|
| كِتَابٌ | سكا يَكِتَبُ | كُتُبٌ |
| دَ ا نِ | يَدَانِ | أَيْدِي |
| مسْلِمٌ | مُسْلِمَانِ | أَمُسْلَمِن |
| قَلَمٌ | يَقْلَمُ | أَقْلَامٌ |
| طِمَنَانِ | فَاطِمَتَانِ | فَاطِمَاتٌ |

Kielelezo 6.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na uwezo mzuri wa uelewa wa maneno katika umoja, uwili na wingi. kama alivyotakiwa, kwani yeye aliweka maneno yasiofahamika kama vitendo au majina ya umoja, uwili ama wingi.

**Kielelezo 6.2 (Kizuri)**



٦ـ أَكْمِلِ الْجَدْوَلَ الْآتِيَةَ:-

| مُفْرَدٌ | مُثَنًّى | جَمْعٌ |
|---|---|---|
| كِتَابٌ | كِتَابَانِ | كُتُبٌ |
| يَدٌ | يَدَانِ | أَيْدِي |
| مسْلِمٌ | مُسْلِمَانِ | مُسْلِمُوْنَ |
| قَلَمٌ | قَلَمَانِ | أَقْلَامٌ |
| فَاطِمَةٌ | فَاطِمَتَانِ | فَاطِمَاتٌ |

Kielelezo 6.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyefanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana alikuwa na uwezo mzuri wa uelewa wa maneno katika umoja, uwili na wingi.kama alivyotakiwa.

### 3.2.4 Swali la 7: Matumizi ya lugha

Swali la sabalilitokana na mada ya herufi ambapo mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa mujibu wa taratibu za lugha ya kiarabu. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa majibu aliyopewa kwa kuzingatia matumizi sahihi ya»حروف رجلا» kwa mujibu wa kanuni na taratibu za lugha husika.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katikamatumizi ya herufi zinazotia kasra neno la mbele yake (حروف رجلا).

Swali lilijibiwa na watahiniwa **3,321** sawa na asilimia **88.82** na watahiniwa **418** sawa na asilimia **11.18** hawakujibu swali hili.Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2d.


**Jadweli nambari 2d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,489 | 74.95 | 542 | 16.32 | 290 | 8.73 | 832 | 25.05 |

Takwimu za jadweli nambari 2d zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa asilimia **74.95** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mbaya kwa asilimia **25.05**. **.**

Aidha, watahiniwa **2,489** sawa na asilimia **74.95** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya matumizi ya ( (حروف رجلا katika sentensi kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1.

**Kielelezo 7.1 (Kibaya)**



٧- ضَعْ حَرْفَ اَلْجَرِّ اَلْمُنَاسِبِ فِيْ اَلْمَكَانِ اَلْخَالِيْ:-

أ- دَخَلَتْ فَاطِمَةُ ____ غُرْفَتِهَا.

ب- ضَرَبَتِ الْأُمُّ وَلَدَهَا ____ اَلْعَصَا.


ج- يَسْقُطُ الثَّلْجُ ____ الْأَرْضِ.

د- يَنْزِلُ الْجُنْدِيُّ ____ الْحِصَانِ.

هـ- ذَهَبَ اَلطَّالِبُ ____ مَدْرَسَتِهِ.

Kielelezo 7.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na uwezo mzuri wala uelewa wa matumizi ya ( (رجلا فورح kwani yeye ameshindwa kutumia ( (رجلا فورح hata moja katika swali hili.

**Kielelezo7.2 (Kizuri)**



٧- ضَعْ حَرْفَ اَلْجَرِّ اَلْمُنَاسِبِ فِيْ اَلْمَكَانِ اَلْخَالِيْ:-

أ- دَخَلَتْ فَاطِمَةُ ____ غُرْفَتِهَا.

ب- ضَرَبَتِ الْأُمُّ وَلَدَهَا ____ اَلْعَصَا.

ج- يَسْقُطُ الثَّلْجُ ____ الْأَرْضِ.

د- يَنْزِلُ الْجُنْدِيُّ ____ الْحِصَانِ.

هـ- ذَهَبَ اَلطَّالِبُ ____ مَدْرَسَتِهِ.

Kielelezo 7.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa ana uwezo mzuri na uelewa wa matumizi mazuri na sahihi ya ((رجلا فورح.

### 3.2.5 Swali la 8:Matumizi ya lugha

Swali la nanelililitokana na mada ya mtenda na mtendwa (لوعفملاو لعافلا) ambapo mtahiniwa alitakiwa kubainisha mtendwa. Swali hili lililikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ﻫ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kubainisha mtendwa kutokana na sentensi alizopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uchambuzi wa sentensi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,428** sawa na asilimia **91.68 na** watahiniwa **311** sawa na asilimia **3.32** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2e


**Jadweli nambari 2e: Uchambuzu wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,087 | 60.88 | 137 | 4.00 | 1,204 | 35.12 | 1,341 | 39.12 |

Takwimu za jadweli nambari 2e zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa asilimia **60.88** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia 39.21. .

Aidha, watahiniwa **2,087** sawa na asilimia **60.88** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya kubaini mtendwa wa kitendo katika sentensi kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.

**Kielelezo 8.1 (Kibaya)**



٨- إِسْتَخْرِجْ اَلْمَفْعُوْلَ بِهِ مِنَ الْجُمَلِ الْآتِيَةِ:-

| اَلْجُمْلَةُ | اَلْمَفْعُوْلُ بِهِ |
|---|---|
| أ- صَنَعَ النَّجَّارُ كُرْسِيًّا. | كلمتن |
| ب- أَكَلَ الْحِمَارُ الْفُوْلَ. | الر فلة |
| ج- حَلَبَتْ الْفَتَاةُ الْبَقَرَةَ. | اَلْحَمَل |
| د- طَبَخَتِ الْمَرْأَةُ الطَّعَامَ. | اَلْمَلَائن |
| هـ - أَبْصَرَ الرَّجُلُ الْهِلَالَ. | اَلْحَجَرِيُّ |

Kielelezo 8.1 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hana uwezo mzuri na uelewa wa utambuzi wa mtenda na mtendwa. Pia inadhihirika kuwa uwezo wake wa uchambuzi wa sentensi

uko chini sana, kwani mtahiniwa huyu alikuja na maeno yake na kuyafanya majibu badala ya kuchukuwa kutoka katika sentensi alizopewa.

**Kielelezo 8.2 (Kizuri)**


٨- إِسْتَخْرِجْ اَلْمَفْعُوْلَ بِهِ مِنَ الْجُمَلِ الْآتِيَةِ:-

| اَلْجُمْلَةُ | اَلْمَفْعُوْلُ بِهِ |
|---|---|
| أ- صَنَعَ النَّجَّارُ كُرْسِيًّا. | كُرْسِيًّا. |
| ب- أَكَلَ الْحِمَارُ الْفُوْلَ. | الفُوْلَ. |
| ج- حَلَبَتْ الْفَتَاةُ الْبَقَرَةَ. | البَقَرَةَ. |
| د- طَبَخَتِ الْمَرْأَةُ الطَّعَامَ. | الطَّعَامَ. |
| هـ - أَبْصَرَ الرَّجُلُ الْهِلَالَ. | الهِلَالَ. |

Kielelezo 8.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa anauwezo mzuri na uelewa wa utambuzi wa mtenda na mtendwa. Pia inadhihirika kuwa uwezo wake wa uchambuzi wa sentensi ni wa kiwango cha juu.

## 3.3 SEHEMU C: KANUNI ZA LUGHA NA SARUFI(القواعد اللغوية)

Katika sehemu hii kulilikuwa na jumla ya maswali manne (04), swali nambari 9,10,11 na 12.Katika mada inayohusu kanuni za lugha. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote ya sehemu hii,ambapo swali la tisa lililikuwa na alama tano (5) , swali la kumi na kumi na moja yalikuwa na alama kumi (10) kila moja na swali la kumi na mbili lililikuwa na alama tano (5). Hivyo jumla ya alama katika sehemu hii zililikuwa ni thalathini.

### 3.3.1 Swali la 9: Kanuni za lugha na Sarufi

Swali la tisa linatokana na mada ya kanuni za lugha na sarufi ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa maana ya Istilahi alizopewa. Swali hili lililikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kutoa au kuleta maana ya Istilahi alizopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa juu ya kanuni za lugha ya kiarabu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,928** sawa na asilimia **78.31** na watahiniwa **811** sawa na asilimia **21.69** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3a.


**Jadweli nambari 3a Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,815 | 61.99 | 414 | 14.14 | 699 | 23.87 | 1,113 | 38.01 |

Takwimu za jadweli nambari 3a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa asilimia **61.99** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **38.01.** .


Aidha, watahiniwa **1,815** sawa na asilimia **61.99** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya utoaji wa maana za istilahi walizopewa, kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1.

**Kielelezo 9.1 (Kibaya)**




Kielelezo 9.1 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hanauwezo wa kueleza maana ya maneno ama istilahi alizotakiwa kuleta maana yake kwani yeye alileta maelezo yasiofahamika na yasiohusiana na mada husika.

**Kielelezo 9.2 (Kizuri)**



٩- عرّف ما يأتي:-

أ- المُبْتَدأ هو اسم مرفوع في أول الجملة.

ب- الحَرْف هو ما لا يظهر معناه كاملا إلا مع غيره.

ج- جَمْعُ التَّكْسِير هو ما دل على أكثر من اثنين أو اثنتين بتغيير صورة مفرده.

د- الفَاعِلُ هو اسم مرفوع تقدمه الفعل ودل على الذي فعل الفعل.

هـ- الضَّمِيرُ هو اسم معرفة تدل على الغائب أو المخاطب أو المتكلم.

Kielelezo 9.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa nauwezo mzuri na uelewa wa kuelezamaana ya maneno ama Istilahi alizotakiwa kuleta maana yake kwa usahihi.

### 3.3.2 Swali la 10: Kanuni za lugha

Swali la kumi lilitokana na mada ya aina za maneno ambapo mtahiniwa alitakiwa kuleta au kuandika kinyume ya maneno aliyopwa. Swali hili lililikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kutoa au kuleta kinyume cha maneno aliyopewa kwa kujaza au kukamilisha maneno hayo katika sehemu zilizoachwa wazi kwa kuzingatia neno na kinyume chake.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika aina za maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,074** sawa na asilimia **82.21** na watahiniwa **665** sawa na asilimia **17.79** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3b.


**Jadweli nambari 3b:Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 3,063 | 99.64 | 9 | 0.29 | 2 | 0.07 | 11 | 0.36 |

Takwimu za jadweli nambari 3b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **99.64** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mbaya kwa asilimia **0.36.** .

Aidha, watahiniwa **3,063** sawa na asilimia **99.64** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada ya aina za maneno kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1.


**Kielelezo 10.1 (Kibaya)**


١٠- هَاتِ أَضْدَادًا لِلْكَلِمَاتِ الْآتِيَةِ:-

| اَلْكَلِمَةُ | ضِدُّهَا |
|---|---|
| أ- جَمِيْلٌ | يَرَان |
| ب- صَعْبٌ | تَقْصَ |
| ج- ثَقِيْلٌ | ثَقِيْلُن |
| د- وَاسِعٌ | وَسِعَ ان |
| هـ- ذَكِيٌّ | ذَكِيْن |

Kielelezo 10.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na maarifa mazuri na uelewa wa kuleta neno na kinyume chake kama alivyotakiwa kufanya. Katika kipengele cha kwanza na cha pili kaleta maneno lakini sio kinyume ya maneno aliyopewa ama kipengele cha tatu, nne na tano kanukuu tu maneno hayohayo na kufanya ni majibu ya maswali husika.

**Kielelezo 10.2 (Kizuri)**


١ - هَاتِ أَضْدَادًا لِلْكَلِمَاتِ الْآتِيَةِ:-

| ضِدُّهَا | اَلْكَلِمَةُ |
|---|---|
| [illegible] | أ- جَمِيْلٌ |
| سَهْلٌ | ب- صَعْبٌ |
| خَفِيْفٌ | ج- ثَقِيْلٌ |
| ضَيِّقٌ | د- وَاسِعٌ |
| غَبِيٌّ | هـ- ذَكِيٌّ |

Kielelezo 10.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa na maarifa mazuri na uelewa wa kuletaneno na kinyume chake kama alivyotakiwa kufanya.

### 3.3.3 Swali la 11:Kanuni za lugha

Swali la kumi na moja lilitokana na mada ya «ينبملاو برعملاو» ambapo mtahiniwa alitakiwa kubainisha maneno yaliyokuwa «ينبم» na yaliyokuwa « برعم».

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwakuweka maneno ambayo ni «ينبم» katika orodha yake na yale ya « برعم» katika orodha yake.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika mada husika. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,556** sawa na asilimia **95.11** na watahiniwa **183** sawa na asilimia **4.89** hawakujibu swali hili.


**Jadweli nambari 3c:Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 474 | 13.33 | 1,755 | 49.35 | 1,327 | 37.32 | 3,082 | 86.67 |

Takwimu za Jadweli nambari 3c zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **13.33** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **86.67** .

Aidha, watahiniwa **474** sawa na asilimia **13.33** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada ya «ينبملا برعملاو» kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.1

**Kielelezo 11.1 (Kibaya)**



١١ - إستخرج من الكلمات الآتية المبنية والمعربة:-


اين — دخل — محمد — كيف — الفلاح — الزهرة — انا — بقرة — أذهب — كتاب

| المعرب | المبني |
|---|---|
| أين | محمد |
| دخل | الفلاح |
| كيف | الزهرة |
| أنا | بقرة |
| أذهب | كتاب |
| | |
| | |

.

Kielelezo 11.1 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na uelewa mzuri na utambuzi wa mada husika kwani ameshindwa kutafautisha ama kubaini kati ya «برعملا»«ينبملا» kama alivyotakiwa kufanya, sababu maneno aliyoyaweka katika orodha ya «ينبملا» yote ni «برعم» na aliyoyaweka katika orodha ya «برعملا» yote ni«ينبم»isipokuwa neno moja tu ndio «برعم».

**Kielelezo 11.2 (Kizuri)**



١١ - إستخرج من الكلمات الآتية المبنية والمعربة:-

اين — دخل — محمد — كيف — الفلاح — الزهرة — انا — بقرة — أذهب — كتاب

| المعرب | المبني |
|---|---|
| أذهب | أين |
| محمد | دخل |
| الفلاح | كيف |
| الزهرة | أنا |
| بقرة | |
| كتاب | |
| | |

Kielelezo 11.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa na uelewa mzuri nautambizi wa mada husika kwani ameweza kutafautisha ama kubaini kati ya «برعملا»«ينبملا» kama alivyotakiwa kufanya.

### 3.3.4 Swali la 12: Kanuni za lugha

Swali la kumi na mbili lilitokana na mada ya kanuni za lugha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa jawabu alizopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kujaza neno litakalokamilisha ibara husika kwa kuchagua jibu au neno sahihi miongoni mwa majibu au maneno aliyopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa na uwezo wa matumizi ya maneno pamoja na umakini wa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa majibu aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,674** sawa na asilimia **98** na watahiniwa **65** sawa na asilimia **1.74** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3d.


**Jadweli nambari 3d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 – 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,382 | 37.61 | 1,108 | 30.16 | 1,184 | 32.23 | 2,292 | 62.39 |

Takwimu za Jadweli na mbari 3d zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **37.62** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wastani kwa asilimia **62.39** .

Aidha, watahiniwa **1,382** sawa na asilimia **37.62** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya uchaguzi wa neno sahihi la kujazwa kulingana na maelezo waliyopewa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.1

**Kielelezo 12.1 (Kibaya)**



١٢- إملأ الفراغات الآتية باختيار كلمة مناسبة مما بين القوسين:-

أ - الأسماء الخمسة ترفع بـ ______ ( الألف ___ الياء ___ الواو).

ب - كل لفظ يدل على حصول عمل في الزمن خاص. ______

( الحرف ___ الفعل ___ الفعل الماضي)


ج - ينصب بالألف نيابة عن الفتحة ______ ( المثنى ___ الأفعال الخمسة ___ الأسماء الخمسة)

د - يرفع اسم وينصب الخبر ______ ( كان ___ ظن ___ كأن)

هـ - لم ولا تجزمان فعلا ______ واحد ( أمرا ___ ماضيا ___ مضارعا)

Kielelezo 12.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hana uelewa mzuri wala maarifa ya kutambua istilahi muafaka kwani hakuweza kuchagua istilahi sahihi au muafaka kulingana na maelezo aliyopewa.

**Kielelezo 12.2 (Kizuri)**



١٢- إملأ الفراغات الآتية باختيار كلمة مناسبة مما بين القوسين:-

أ - الأسماء الخمسة ترفع بـ ______ ( الألف ___ الياء ___ الواو).

ب - كل لفظ يدل على حصول عمل في الزمن خاص. ______

( الحرف ___ الفعل ___ الفعل الماضي)

ج - ينصب بالألف نيابة عن الفتحة ______ ( المثنى ___ الأفعال الخمسة ___ الأسماء الخمسة)

د - يرفع اسم وينصب الخبر ______ ( كان ___ ظن ___ كأن)

Kielelezo 12.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeweza kufanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa na uelewa mzuri na maarifa ya kutambua istilahi muafaka kwani aliweza kuchagua istilahi sahihi au muafaka kulingana na maana au maelezo aliyopewa.

## 3.4. SEHEMU D: UTUNGAJI(التعبير))

Sehemu hii ililikuwa na maswali mawili (02) yanayohusu uandishi. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swalimoja (1) tu katika sehemu hii, ambapo kila swali lililikuwa na alama 20.

### 3.4.1 Swali la 13: Utungaji

Swali la kumi na tatu lilitokana na mada ya utungaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kuandika au kutunga insha kwa mujibu wa vigezo sahihi na vinavyo kukubalika katika uandishi. Hivyo mtahiniwa alipaswa kuzingatia yafuatayo:

1. Kutoa hoja za kimantiki na zinazokubalika katika utungaji wa insha.
2. Kufuata utaratibu sahihi na unaokubalika katika uandishi wa insha.
3. Kufuata mtiririko au mshikano wa matukio au hoja.
4. Kuepukana na makosa ya kilugha ama kiuandishi au muundo.
5. Kuzingatia utangulizi, madhumuni na kifungio.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa utungaji wa insha kwa mujibu wa mada aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,813** sawa na asilimia **48.49** na watahiniwa **1,926** sawa na asilimia **51.51** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4a.


**Jadweli nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4.5 | | 5–12.5 | | 13 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,606 | 88.58 | 155 | 8.55 | 52 | 2.87 | 207 | 11.42 |

Takwimu za jadweli nambari 4a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **88.58** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mbaya kwa asilimia **11.42.**


Aidha, watahiniwa 1,606 sawa na asilimia 88.58 wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya utungaji wa insha kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 13.1.

**Kielelezo 13.1 (Kibaya)**


١٣- تَحَدَّثْ عَنْ فَائِدَةِ طَلَبِ الْعِلْمِ فِي الْحَيَاةِ.

Kielelezo 13.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alijibu swali hili kwa kuandika bila kufuata taratibu na kanuni za uandishi na utungaji wa insha bali aliandika maelezo yasiofahamika.


**Kielelezo13.2 (Kizuri)**



١٣- تَحَدَّثْ عَنْ فَائِدَةِ طَلَبِ الْعِلْمِ فِي الْحَيَاةِ.

ج١٣ "طَلَبِ الْعِلْمِ فِي الْحَيَاةِ"

الْعِلْمُ هُوَ مِفْتَاحٌ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ فِي
هَذِهِ حَيَاةِ الدُّنْيَا، وَأَيْضًا، الْعِلْمُ نُورٌ
فِي الْمَائِدَةِ أَوِ الْحَيَاةِ، كُلُّ مُسْلِمٍ وَجَبَ
عَلَيْهِ أَوْ عَلَيْهَا أَنْ يَطْلُبَ الْعِلْمَ.
الْعِلْمُ سَبَبٌ أَنْ تَعْرِفَ رَبَّكَ
وَعِبَادَتَهُ صَحِيحًا كَمَا قَالَ فِي كِتَابِهِ
الشَّرِيفِ (الْقُرْآنِ) فِي كَثِيرِ الْآيَاتِ.
فَوَائِدُ الْعِلْمِ كَثِيرَةٌ كَمَا يَلِي:
الْعِلْمُ سَبَبٌ وَظِيفَةِ التَّدْرِيسِ،
شَيْخٌ، قَاضٍ، الْإِمَامُ، مُعَلِّمَاتٌ، مُعَلِّمٌ،
الدُّكْتُورُ، الْفَلَّاحُ، حَاكِمٌ، رَئِيسٌ.
وَهَكَذَا كَثِيرًا.


أيضًا العلمُ، سببٌ أنْ تُعرفَ القرآن كتبدا
تفاسير القرآن، وأيضًا تجدُ الفلوس
كثيرة، العلمُ تُخرجُ المساكين و
الفقراءَ وكلَّ حال نتعلم، عندما نطلبُ العلمَ
بلا العلمِ، سترجدُ المسكين، الفقراءُ،
المجنونُ، مجهولٌ، التفيهة، كالذي
الزاني، السارقُ، وظالمٌ كبيرًا.
لذلك، تجبُ علينا أن نطلبَ العلمَ
نجدُ كلَّ فائدة، ونعلمُ أخرى عن بعدنا

Kielelezo 13.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alijibu swali hili kwa kuandika na kufuata taratibu na kanuni za uandishi na utungaji insha.

### 3.4.2 Swali la 14: Utungaji

Swali la kumi na nne lilitokana na mada ya utungaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kuandika au kutunga makala kwa mujibu wa vigezo sahihi na vinavyo kukubalika katika uandishi huo. Hivyo mtahiniwa alipaswa kuzingatia yafuatayo:

1. Kutoa hoja za kimantiki na zinazokubalika katika utungaji wa nakala.
2. Kufuata utaratibu sahihi na unaokubalika katika uandishi wa nakala.
3. Kufuata mtiririko au mshikano wa matukio au hoja.
4. Kuepukana na makosa ya kilugha ama kiuandishi au muundo.
5. Kuzingatia utangulizi, madhumuni na kifungio.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa utungaji wa makala kwa mujibu wa mada aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **250** sawa na asilimia **6.69** na watahiniwa **3,489** sawa na asilimia **93.31** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4b.


**Jadweli nambari 4b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4.5 | | 5–12.5 | | 13 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 235 | 94.00 | 12 | 4.80 | 3 | 1.20 | 15 | 6.00 |

Takwimu za jadweli nambari 4b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **94.00** upokatikakiwangocha vibaya ambapoumepelekeaufauluwa jumla kuwa mbaya kwaasilimia **6.00.**


Aidha, watahiniwa **235** sawa na asilimia **94.00** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya uandishi na utungaji wa makala kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 14.1.

**Kielelezo 14.1 (Kibaya)**


١٤ - تحدث عن أهمية حقوق الوالد.

Kielelezo 14.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alijibu swali hili kwa kuandika bila kufuata taratibu na kanuni za uandishi na utungaji wa makala bali pia maelezo yake hayafahamiki.

**Kielelezo14.2 (Kizuri)**



١٤- تحدث عن أهمية حقوق الوالد.

حق الولد على والده.

Kielelezo 14.2 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alijibu swali hili kwa kuandika na kufuata taratibu na kanuni za uandishi na utungaji wa makala.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali matatu yalijibiwa vizuri, maswali saba yalijibiwa wastani na maswali manne yalijibiwa vibaya.

Uchambuzi huu unaonesha kuwa, ili ufaulu uwe mzuri na wa ufanisi hutokana na jitihada za watahiniwa wenyewe katika kufahamu matakwa ya swali husika, maarifa waliyo nayo juu ya mada husika na kuwa na uelewa mzuri wa lugha ya Kiarabu.

Pia watahiniwa wengi hawakujibu vizuri maswali kutokana na kutokuwa na uelewa mzuri wa matakwa ya maswali, kukosa maarifa juu ya mada zilizojitokeza katika mtihani, kutokuwa na msamiati wa kutosha wa lugha ya Kiarabu, jambo ambalo liliwafanya washindwe kujieleza kwa kutumia lugha hiyo. Bali wapo watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuandika lugha ya Kiarabu.

Taarifa hii itasaidia kunyanyua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiarabu na kutoa changamoto kwa walimu, wanafunzi na wadau wote katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Lengo likiwa ni kukuza lugha ya Kiarabu na kufanya marekebisho ya dosari mbalimbali zilizojitokeza mwaka 2023 na kupelekea kuongeza ufaulu katika mitihani mingine inayofuata.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kupitia uchambuzi huu mapendekezo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa ili kuinua kiwango cha ufaulu:-

a) Walimu wazingatie muhtasari wa somo wanapofundisha mada mbalimbali.

b) Wanafunzi wahamasishwe katika kulishughulikia somo la Kiarabu kwa sababu linaweza kuwapatia fursa nyingi za kujiajiri katika maisha yao iwapo watafaulu vizuri.

c) Walimu watoe mazoezi mengi kadiri inavyowezekana kwa wanafunzi ili kuwapa na kuwajenga uwezo wa kuelewa na kujibu maswali ya mtihani kulingana na matakwa ya kila swali.

d) Wakaguzi, walimu wakuu na wakuu wa seksheni waendelee kuwasimamia walimu wa somo la Kiarabu ili kuhakikisha wanakamilisha muhtasari kwa wakati na wanatimiza kazi zao za ufundishaji ipasavyo.

e) Washauri wazidishe bidii na mkazo zaidi katika kuwapa msaada stahiki walimu ili kuhakikisha kwamba dosari za ufundishaji zinapatiwa utatuzi madhubuti, hasa kwa zile mada ambazo ufaulu wake umebainika kuwa ni wa kiwango cha chini.

f) ) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar kwa kupitia Taasisi ya Elimu Zanzibar ihakikishe inaandaa na kusimbaza vitabu vya kiada

na ziada kwa wanafunzi wanaosoma somo la lugha ya Kiarabu. Pamoja na kuwapatia walimu vitabu rejea vinavyoendana na muhtasari wa somo lenyewe.

g) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Elimu ya Zanzibar ifanye jitihada za makusudi katika kuwapatia mafunzo walimu wa somo hili. Vilevile kulishajihisha somo hili sawa na yanavyoshajihishwa masomo mengine ya lugha kama Kiswahili na Kiingereza.

h) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Zanzibar iandae utaratibu wa kuwafunza walimu namna bora za utunzi wa maswali ili walimu hao wawe na uwezo mzuri wa kuwaandaa wanafunzi kuukabili mtihani wa taifa.

i) Vyuo vya ualimu navyo vihakikishe vinawaandaa vyema walimu ili kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazolikabili somo hili.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO NAMBARI I

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA

### MWAKA 2023

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KANUNI ZA LUGHA | 11 | 88.67 | VIZURI |
| 2 | UFAHAMU | 2 | 85.90 | VIZURI |
| 3 | MATUMIZI YA LUGHA | 6 | 64.51 | VIZURI |
| 4 | KANUNI ZA LUGHA | 12 | 62.39 | WASTANI |
| 5 | MATUMIZI YA LUGHA | 5 | 58.54 | WASTANI |
| 6 | UFAHAMU | 3 | 55.65 | WASTANI |
| 7 | UFAHAMU | 1 | 54.38 | WASTANI |
| 8 | MATUMIZI YA LUGHA | 8 | 39.12 | WASTANI |
| 9 | KANUNI ZA LUGHA | 9 | 38.01 | WASTANI |
| 10 | MATUMIZI YA LUGHA | 4 | 35.44 | WASTANI |
| 11 | MATUMIZI YA LUGHA | 7 | 25.05 | VIBAYA |
| 12 | UTUNGAJI | 13 | 11.42 | VIBAYA |
| 13 | UTUNGAJI | 14 | 6.00 | VIBAYA |
| 14 | KANUNI ZA LUGHA | 10 | 0.36 | VIBAYA |

## KIAMBATANISHO NAMBARI 2

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKAS 2022

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UFAHAMU | 2 | 83.21 | VIZURI |
| 2 | UFAHAMU | 3 | 59.25 | WASTANI |
| 3 | KANUNI ZA LUGHA | 11 | 35.60 | WASTANI |
| 4 | MATUMIZI YA LUGHA | 6 | 21.93 | VIBAYA |
| 5 | MATUMIZI YA LUGHA | 4 | 18.09 | VIBAYA |
| 6 | KANUNI ZA LUGHA | 9 | 14.79 | VIBAYA |
| 7 | MATUMIZI YA LUGHA | 8 | 13.74 | VIBAYA |
| 8 | MATUMIZI YA LUGHA | 5 | 13.12 | VIBAYA |
| 9 | MATUMIZI YA LUGHA | 7 | 12.90 | VIBAYA |
| 10 | UFAHAMU | 1 | 11.16 | VIBAYA |
| 11 | KANUNI ZA LUGHA | 12 | 8.29 | VIBAYA |
| 12 | UTUNGAJI | 13 | 2.49 | VIBAYA |
| 13 | KANUNI ZA LUGHA | 10 | 2.19 | VIBAYA |
| 14 | UTUNGAJI | 14 | 0.56 | VIBAYA |